TANGAZO LA SERIKALI NA. 554 La Tarehe 26/07/2019.

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 28(1)(d))*

AMRI YA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NJOMBE ("NJOMBE WSSA"), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii litajulikana kama, Amri ya Marekebisho ya Bei ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe("Njombe WSSA") ya Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa kuanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi za Njombe WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 30 Septemba 2019 au kabla, Njombe WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hiyo;

(b) Njombe WSSA itahakikisha imewafungia dira wateja wote ifikapo Juni 2021;

(c) Njombe WSSA itahakikisha inaandaa na kutekeleza programu ya usawa na uwazi ya mgawo wa maji kwa wateja wote wanaoathirika na mgao;

(d) ifikapo Juni 2022 Njombe WSSA ianzishe mpango wa kutibu majitaka;

(e) Njombe WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(f) Njombe WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(g) Njombe WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa; na

(h) Njombe WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za

fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Njombe WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Njombe WSSA katika siku zijazo.

Kufutwa kwa Amri Na. 015-020

5. Amri hii linafuta matumizi ya Amri Na. 015-020 ya 28 Oktoba 2015 katika maeneo yanayohudumiwa na Njombe WSSA

JEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali la 1(a): Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa kwa wateja wenye dira (Shilingi/ mita ya ujazo)

| Kundi la wateja | Matumizi | Bei za sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 0-5 uniti | 900 | 1,460 | 1,680 | 1,740 |
| | 6-10 uniti | 980 | 1,590 | 1,830 | 1,900 |
| | >11 uniti | 1,000 | 1,630 | 1,870 | 1,940 |
| Taasisi | 1-5 uniti | 1,000 | 1,630 | 1,870 | 1,940 |
| | 6-10 uniti | 1,100 | 1,790 | 2,060 | 2,130 |
| | >10 uniti | 1,150 | 1,870 | 2,150 | 2,230 |
| Biashara | | 1,100 | 1,790 | 2,060 | 2,130 |
| Viwanda | | 1,100 | 1,790 | 2,060 | 2,130 |
| Magati | | 1,000 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| Wastani wa uwiano | | 995 | 1,616 | 1,859 | 1,927 |

Jedwali la 1(b): Bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa kwa wateja wasio na dira (Shilingi/mwezi)

| Kundi la wateja | Bei za sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 13,650 | 15,650 | 17,950 | Haijaidhinishwa |

Jedwali la 1(c): Tozo ya huduma ya sasa na iliyoidhinishwa (Shilingi/mwezi)

| Kundi la wateja | Tozo ya Sasa | Tozo iliyoidhinishwa |
|---|---|---|
| | Mpaka Machi 2018 | Kutoka tarehe 1 Aprili 2018 na kuendelea |
| Majumbani | 3000 | Hairuhusiwi |
| Taasisi | 4000 | |
| Biashara | 4000 | |
| Viwanda | 4000 | |

Jedwali la 1(d): Ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya maunganisho ya maji safi (Shilingi/maunganisho)

| Kundi la wateja | Ada za sasa | Ada zilizoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 – 2021/22 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya vifaa ya maunganisho mapya na nguvu | Asilimia 20 ya vifaa ya maunganisho mapya na nguvu kazi kama |
| Taasisi | | |

*Tangazo La Serikali Na. 540 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| Biashara | kazi kama ilivyoidhinishwa katika Kanuni za Majiza Mwaka 2013 | ilivyoidhinishwa katika Kanuni za Maji zaMwaka 2013 |
| Viwanda | | |

Jedwali la 1(e): Ada ya sasa na iliyoidhinishwa ya kurejeshewa huduma ya maji baada ya kukatiwa (Shilingi/kurejeshewa huduma)

| Kundi la Wateja | Ada za sasa | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 20,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 25,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 25,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 25,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

________

JEDWALI LA PILI

________

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZA NDANI ZA NJOMBE WSSA (MILIONI ZA SHILINGI ZA KITANZANIA)

| Maelezo | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|
| Ukarabati na ubadilishaji wa vifaa | | | | |
| | Chanzo cha maji cha Magoda: kuongeza ukuta wa ukingo wa chanzo, kuongeza kidakamaji, kubadilisha sluice valvu chenye inchi 8 na kujenga chemba ya dira kubwa ya maji | 0.00 | 15.00 | 0.00 |
| | Chanzo cha maji cha Lunyanywi: kuongeza kidakamaji, kubadilisha chujio, kujenga chemba ya dira kubwa ya maji na kubadilisha njia ya maji yaliyozidi kwenye chanzo (spillway) yenye geti cha chuma | 1.00 | 2.50 | 0.50 |
| | Chanzo cha maji cha Wikichi: kuongeza ukuta wa ukingo wa chanzo, kuongez akidakamaji, kubadilisha sluice valvu chenye inchi 6 na kujenga chemba ya dira kubwaya maji | 1.50 | 3.00 | 2.00 |
| | Chanzo cha maji cha kusukuma maji kwa kutumia umeme cha Kibena Howard: kutengeneza eneo la chanzo na kujenga uzio | 7.50 | 20.00 | 7.50 |
| | Kubadilisha dira mbovu 670 zenye ukubwa wa inchi ¾ | 4.47 | 28.14 | 31.52 |
| Jumla ndogo ya gharama za ukarabati na ubadilishaji wa vifaa | | 14.47 | 68.64 | 41.52 |
| Miradi mipya | | | | |
| | Kununua gari jipya aina ya Toyota Pick-up Double Cabin | 0.00 | 0.00 | 115.00 |
| | Kununua pikipiki 9: 2 mwakawa kwanza, 3 mwaka wa pili na 4 mwaka watatu | 6.00 | 9.00 | 12.00 |
| | Kununua mabomba na na viungio kwa ajili ya kuongeza mtandao wa majimaeneo ya Kambarage kwa umbali wa kilomita 8 ifikapo Juni 2022 | 15.00 | 70.00 | 94.39 |

*Tangazo La Serikali Na. 540 (Linaendelea.)*

| Maelezo | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|
| | Kununua mabomba na naviungio kwa ajili ya kuongeza mtandao wa majima eneo ya uwanja wa ndege kwa umbali wa kilomita 5 ifikapo Juni 2022 | 14.00 | 40.00 | 72.00 |
| | Kununua mabomba na naviungio kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maj imaeneo ya Igereke kwa umbali wa kilomita 5 ifikapo Juni 202 | 15.00 | 50.00 | 86.00 |
| | Kununua mabomba na naviungio kwa ajili ya kuongeza mtandao wa majima eneo ya Kilimani about 7km by June,2022 | 15.00 | 51.78 | 84.00 |
| | Kununua na kuweka dira za maji 1200 zenye ukubwa wa inchi 3/4" kwa wateja wasio nadira | 58.08 | 56.28 | 0.00 |
| | Kununua dira za maji 1500 kwa wateja wapya, 500 kila mwaka. | 44.65 | 46.90 | 49.25 |
| | Kununua dira za malipo ya kabla; 30 pamoja na viungio vyake kwa ajili ya wateja wa taasisi na biashara | 0.00 | 4.63 | 7.29 |
| | Kununua na kuweka vifaa vya kuua vijidudu (Chlorine dosing facility) katika chanzo cha Kibena Howard | 20 | 0 | 0 |
| | Kununua samani na vifaa vya ofisi | 0 | 13 | 1 |
| Jumla ndogo ya gharama za uwekezaji mpya | | 187.73 | 341.59 | 520.93 |
| Jumla ya ghamarazauwekezaji. | | 202.20 | 410.23 | 562.45 |

JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

| Kiashiria | Kipimo | Lengo la utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Namba ya wateja wapya | Na. | 500 | 500 | 500 |
| Upotevu wa Maji | % | 30 | 29 | 28 |
| Ufanisi wa ukusanywaji wa mapato (bila madeni) | % | 87 | 90 | 92 |

JEDWALI LA NNE

*Tangazo La Serikali Na. 540 (Linaendelea.)*

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (Milioni TZS)

| Gharama | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| | Iliyoidhinishwa | Iliyoidhinishwa | Iliyoidhinishwa |
| Uzalishaji | 57.62 | 60.77 | 64.27 |
| Umeme | 59.51 | 89.26 | 119.01 |
| Usambazaji | 117.53 | 44.79 | 62.04 |
| Matengenezo | 33.42 | 39.16 | 40.06 |
| Watumishi | 681.25 | 725.46 | 769.83 |
| Utawala | 428.16 | 646.51 | 694.46 |
| Matangazo | 16.60 | 17.52 | 19.62 |
| Matukio | 48.37 | 53.95 | 60.28 |
| Bodi | 171.68 | 241.54 | 277.77 |
| Fedha | 2.22 | 2.55 | 2.94 |
| Jumla ya gharama za uendeshaji na matengenezo | 1,616.36 | 1,921.52 | 2,110.28 |
| Uchakavu | 199.10 | 357.75 | 484.96 |
| FaidayaUwekezaji | 3.11 | 52.48 | 77.49 |
| Jumla ya mahitaji ya fedha | 1,818.56 | 2,331.75 | 2,672.74 |
| Kutoa mapato mengineyo | 21.23 | 21.88 | 25.01 |
| Jumla ya mahitaji ya fedha yanayotokana na mauzo ya maji | 1,797.32 | 2,309.87 | 2,647.72 |

Dodoma NZINYANGWA E. MCHANY

..................................... 2019 *Mkurugenzi Mkuu*